



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



*Urapujuvu tafadhali taja:*

KUMB.NA.NA. IMC/CE/5/2/88

02 Agosti, 2024

### TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Kwa madhumuni ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 12 (1) (b) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Tangazo la Serikali Na.389 la tarehe 17/5/2024, Afisa Mwandikishaji wa Jimbo la Ilemela, anawataarifu waombaji wote walioomba nafasi za kazi za muda za **Waandishi Wasaidizi** na **Waendeshaji** wa Vifaa vya Bayometriki kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kuwa usaili wa nafasi hizo utafanyika tarehe **5 Agosti 2024** katika **Shule ya Sekondari Buswelu** kuanzia saa **6.00 Mchana**.

#### Mambo ya kuzingatia kwa wasailiwa wote:-

1. Usaili utafanyika tarehe **5 Agosti 2024** katika **Shule ya Sekondari Buswelu**. Kuanzia saa **6.00 Mchana**.
2. Kila msailiwa anapaswa kuwa na **kitambulisho** kwa ajili ya utambuzi
3. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na kitambulisho cha NIDA, kitambulisho cha Mpiga Kura, Hati ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa.
4. Kila msailiwa atajigharamia chakula, usafiri na malazi.
5. Kila msailiwa anapaswa kuzingatia tarehe, muda na mahali pa usaili.

6. Kila msailiwa anapaswa kuja na kalamu (pen) ya rangi ya bluu/nyeusi kwa ajili ya kuandikia
7. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia masharti yatakayowekwa.

Orodha ya wanaoitwa kwenye usaili imeambatishwa na tangazo hili.

Limetolewa na:-

  
Ummy M. Wayayu  
**AFISA MWANDIKISHAJI**  
**JIMBO LA ILEMELA**